



Hakika mimi sikutumwa kuwa mtoa laana, bali nilitumwa kuwa huruma

Kutoka kwa Abuu Huraira radhi za Allah ziwe juu yake amesema: Palisemwa: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu waombe dua mbaya washirikina, akasema: "Hakika mimi sikutumwa kuwa mtoa laana, bali nilitumwa kuwa huruma".

[Sahih] [Imepokelewa Imamu Muslim]

Alitakwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake awaombe washirikina dua mbaya kwa Mwenyezi Mungu, akasema: Hakika mimi sikuagizwa na Mwenyezi Mungu na sikutumwa kuwa mtoa laana na kuwaombea watu kuwekwa mbali na rehema ya Mwenyezi Mungu na niwakatie heri, mimi sikutumwa kwa hayo, bali nilitumwa niwe sababu ya heri na rehema kwa watu wote, na kwa waumini hasa.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/66272>

النجاة الخيرية
ALNAJAT CHARITY

